# UJUMBE WA MWANDISHI

Watu wote wanahitaji mahusiano bora na mahusiano mazuri ni haki yako tangu ulipozaliwa. Mungu anataka uwe na mahusiano mazuri, lakini kuanzisha mahusiano huwa ni mchakato unaoanza na mvuto, kufahamina kisha maamuzi.

Unahitaji kumfahamu mtu kihaiba ili uweze kuhusiana naye vizuri, ukimfahamu mwenzako itakusaidia kujua uwezo wake na udhaifu wake.

Kwasababu kwenye mahusiano kuna umuhimu wa kuchukuliana! Utaweza kumchukulia mtu ambaye unamfahamu maeneo yake aliyo na udhaifu.

Jiandae kumfahamu mwenzako! kwa sababu umeamua kuanza safari hiyo ya kumfahamu kwa kusoma kitabu hiki cha haiba ya mtu na jinsi ya kuhusiana naye.

Siyo kwa bahati mbaya kwamba kitabu hiki sasa kipo mkononi mwako, mshukuru Mungu kisha endelea kukisoma bila kuruka vipengele vyake.

# YALIYOMO

Shukrani…………………………………………………..........5
Utangulizi………………………………………….........7

## SURA YA KWANZA

Haiba ni nini?...........................................................10
Umuhimu wa kufahamiana kihaiba. …………………15

## SURA YA PILI

Haiba ya mtu na jinsi ya kuhusiana naye……………..18
Sangwini………………………………………………..20
Koreliki…………………………………………………28
Melankoli ………………………………………………43
Fregmatiki……………………………………………...58
Je, kila mtu ana haiba moja au zaidi?...........................71
Ufafanuzi kuhusu kuwa na haiba mbili………….. ......76
Je, unaweza kuhusiana na haiba yoyote?......................84
Jitathimini na ugundue haiba yako……………………89

## SURA YATATU

Ulianzisha mahusiano yako vibaya……………………97
Humfahamu mwenzako………………………………102
Unashindana na mwenzako………………………...104
Hamuombi pamoja……………………………………..106
Je, unaweza kuibadilisha tabia ya mme au mke wako?...........................................................................109
Hitimisho……………………………………………...110
Kuhusu mwandishi……………………………………111

## SHUKRANI

Furaha yangu ni kuona watu wamefanikiwa katika maisha yao na kuishi maisha yenye furaha na amani. Namshukuru mwenyezi Mungu ambaye amekuwa mwema kwa kuniwezesha kukifikisha kitabu hiki mikononi mwako. Ilikuwa ni shauku yangu kufanya kitu kwa ajili ya kuongeza thamani kwenye maisha yako kupitia kukupa maarifa kisha uyaboreshe mahusiano yako kwa maarifa hayo.

Nimejawa na shukrani sana maana naamini kwamba kitabu hiki utakisoma kwa lengo la kujifunza na kupata maarifa yatakayo kuwezesha kuwa bora kwenye mahusiano yako.

Wengi wamehusika katika kufanikisha uandishi wa kitabu hiki, ndugu zangu, marafiki na jamaa zangu wote mchango wao umefanikisha kukamilika kwa kitabu hiki. Bila kutaja majina yao na nafasi zao kwangu nipende kusema nawashukuru sana kwa kufanikisha kazi hii iliyo njema. Msomaji wangu nakushukuru sana kwa kufanya maamzi ya kupata hiki kitabu ili uweze kujiongezea maarifa. Asante kwa

kuipokea huduma hii ambayo Mungu ameiweka ndani yangu kwa ajili yako.

Nitakuwa na shukrani maalumu kwa ajili yako endapo utanipa mrejesho wako baada ya kupata kitabu hiki ukakisoma na kukimaliza.

Furaha nitakayo isikia ndani yangu itanisukuma kuwa na shukrani za kikepee kwako wewe kama msomaji mwenye nia ya dhati ya kujifunza na kuithamini kazi hii ambayo Mungu ameileta kwangu kama zawaidi kwa ajili ya wengine.

Nakutakia Baraka za Mungu katika kusoma na kufanyia kazi maarifa ya kitabu hiki.

Karibu na uwe na usomaji mwema!

Baada ya kumaliza kusoma kitabu hiki, unaweza kumshirikisha na mwenzako ili ajenge upya msingi wa maisha yake ya kimahusiano.

# UTANGULIZI

Watu wote ni sawa ukizingatia masuala ya haki za binadamu na misingi ya kisheria. Kwa mjibu wa katiba ya jamuhuri ya muungano wa Tanzania, ibara ya kumi na mbili kipengele kidogo cha kwanza inasema kwamba “binadamu wote huzaliwa **huru** na wote ni **sawa**” katika kipengele kidogo cha pili cha ibara hiyo hiyo inasema kwamba “ watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria”.

Lakini watu hao hao huwa wanatofautiana kihaiba, kwahiyo kwa kuzingatia masuala ya haiba za watu, binadamu huwa wanagawanyika katika makundi tofauti tofauti ya kihaiba.

Katika kujifunza na kuongeza maarifa sahihi ya kimahusiano ili kuweza kuyaboresha na kuyafurahia mahusiano yako. Kuna umuhimu mkubwa sana wa kuzifahamu tofauti za watu kihaiba, maana kuzijua haiba za watu inasaidia kujua namna ya kuhusiana au namna ya kuishi na mtu kulingana na haiba yake.

Kupitia kitabu hiki tunakwenda kuchambua haiba za watu na kuona namna au njia iliyo bora ya kuhusiana na kila haiba pamoja na namna bora ya kuishi na mtu kwa mjibu wa haiba

yake. Itakuwa ya faida sana ukifanyia kazi maarifa ambayo yamesheheni katika kitabu hiki.

Tunaweza kupunguza migogoro kwa kiwango kikubwa ambayo inatokea katika jamii endapo watu wote wakifanikiwa kufahamiana kwa misingi ya haiba. Kila mmoja akifahamu kwa kina udhaifu wa mwenzake na uwenzo wa mwenzake inaweza kuwa rahisi sana kudumisha amani katika jamii.

Kabla hujaendelea kusoma kitabu hiki jiulize, Je wewe ni mtu wa haiba gani?

Unaweza kuendana sana na haiba gani?

Kama umeshindwa kujibu maswali hayo basi wewe ni miongoni mwa watu ambao kitabu hiki kitawasaidia sana.